TANGAZO LA SERIKALI NA. 912 la tarehe 16/10/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

SURA 290

# SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya Bunda ya Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri ya kufanya shughuli yoyote iliyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

"maeneo maalumu" inajumuisha maeneo yaliyopimwa au yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanyia shughuli maalum;

"mazao ya uvuvi" maana yake ni samaki, dagaa, magamba ya samaki, makasha ya konokono au malighafi yoyote inayotokana na shuguli za uvuvi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

'ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"utamaduni" maana yake ni shughuli za muziki,

maigizo, mazingaombwe, sinema na michezo;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa ada na ushuru wa mazao ya majini, viwandani na kilimo

3.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya shughuli zinazofanyika katika eneo la Halmashauri na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Kibali cha Kusafirisha bidhaa

5. Kila mtu atakayesafirisha mazao zaidi ya tani moja toka Halmashauri kwenda nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali cha kusafirisha mazao, kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Kizuizi

6 Halmashauri inaweza kuweka kizuizi katika eneo lolote ndani ya eneo la Halmashauri kwa ajili ya

. kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Ushuru kwa wafanyabiashara na watoa huduma wadogo

7. Kila Mfanyabiashara mwenye kitambulisho cha wafanyabiashara na watoa huduma wadogo kilichotolewa na selikali hatatozwa ushuru wa aina yoyote katika biashara yake ambayo ilikidhi vigezo vinavyotakiwa kuwa na kitambulisho hicho.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

8.-(1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

9.-(1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ada na ushuru.

(3 Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo

) cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

10.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa wakati wa muda wa kazi anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

1 ( Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa

na adhabu

2.-(1) endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufililisha kosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum na kulipa ada au ushuru anaodaiwa kama iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 410 la Mwaka 2012

14. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda za Mwaka 2012.

JEDWALI LA KWANZA

*(limetengenezwa chini ya kifungu cha 3(1))*

SEHEMU 'I' Ushuru wa mazao ya kilimo

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Pamba | 3% ya bei |
| 2 | Mahindi | 3% ya bei |
| 3 | Mpunga | 3% ya bei |
| 4 | Mihogo au Viazi | 3% ya bei |
| 5 | Ulezi,Uwele,Mtama | 3% ya bei |
| 6 | Maharage au jamii ya maharage | 3% ya bei |
| 7 | Maembe au tikiti maji | 3% ya bei |
| 8 | Alizeti | 3% ya bei |
| 9 | Karanga au mchele | 3% ya bei |
| 10 | Dengu, choroko | 3% ya bei |
| 11 | Nyanya | 3% ya bei |
| 12 | Vitunguu | 3% ya bei |
| 13 | Mazao mengine ambayo hayajabainishwa | 3% ya bei |

SEHEMU 'II' Ushuru wa mazao ya uvuvi

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Samaki wabichi | Kilo moja | 3% ya bei |
| 2 | Samaki wakavu | (i) tenga dogo la kg 0-20 | Halilipiwi |
| | | (ii) tenga la saizi ya kati la kg 21-50 | Tshs 5,000/= |
| | | (iii) tenga kubwa la kg 51-100 | Tshs 10,000/= |
| | | (iv) kwa kila kilo inayoongezeka zaidi ya kg 100 | Tshs 500/= |
| 3 | Dagaa | (i) gunia la dagaa lenye kg 1-20 | Halilipiwi |
| | | (ii) gunia la dagaa lenye kg 21-50 | Tshs 2,000/= |
| | | (iii) gunia la dagaa lenye kg 51-100 | Tshs 3,000/= |
| | | (iv) kwa kila kilo inayoongezeka zaidi ya kilo 100 | Tshs 200/= |
| 4 | makasha ya konokono | (i) gunia la kg 1-20 | Tshs 1000/= |
| | | (ii) gunia la kg 21-50 | Tshs 2000/= |
| 5 | chakula cha mifugo | (i) gunia lenye kg 1-20 | Halilipiwi |
| | | (ii) gunia lenye kg 21-50 | Tshs 2,000/= |
| | | (iii) gunia lenye kg 51-100 | Tshs 3,000/= |
| | | (iv) kwa kila kilo | Tshs 200/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | inayoongezeka zaidi ya kilo 100 | |
| 6 | Mabini ya samaki | | Tshs 20,000/= kwa mwezi |

SEHEMU 'III' Ushuru wa mazao ya misitu

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa gunia lenye kilo 1-50 | Tshs.2000/= |
| | Mkaa gunia lenye kilo 51-100 | Tshs. 4000/= |
| 2. | Ushuru wa mbao kwa ubao mmoja | Tshs.100/= |
| 3. | Ushuru wa kuni zilizopakiwa kwenye gari la tani 1-7 | Tshs. 20,000/= |
| 4. | Ushuru wa mzigo wa kuni uliowekwa kando ya barabara au unauzwa sokoni kila mzigo mmoja | Tshs. 200/= |
| 5. | Ushuru wa nguzo moja ya mti | Tshs. 200/= |
| 6. | Ushuru wa asali inayouzwa nje ya Wilaya kwa lita 1 | Tshs.50/= |

SEHEMU 'IV': Ushuru wa maegesho ya mitumbwi na boti za kusafirishia abiria

1. Mitumbwi ya kusafirisha abiria……………………Tshs 2,000/= kwa siku
2. Boti za abiria……………………………………… Tshs 3,000/= kwa siku

SEHEMU 'V': Ushuru wa maegesho ya magari kwenye maeneo ya biashara

1. Gari lenye tani 1-3…… 1,000/= kwa siku
2. Gari lenye tani 4-7……. 1,500/= kwa siku
3. Gari lenye tani 7-10…… 2,000/= kwa siku
4. Gari la zaidi ya tani 10… 5,000/= kwa siku

SEHEMU 'VI': Ada ya maegesho ya pikipiki za biashara

1. Pikipiki ………………………10,000/= kwa Mwaka

SEHEMU 'VII': Ada ya shughuli za utamaduni

1. Kibali cha kuchezesha disco, maonyesho ya bendi, Sanaa za maonyesho (maigizo, mazingaombwe, sinema na video kwa vikundi vya ndani ya Wilaya) Tsh. 50,000/= kwa mwaka.

SEHEMU 'VIII': Ushuru wa kuchinja mifugo

| Mfugo | Kiwango cha ushuru |
|---|---|
| Ng'ombe | 3,000/= |
| Mbuzi | 1,300/= |
| Nguruwe | 1,300/= |
| Kondoo | 1,300/= |

SEHEMU 'IX': Ada za vibali vya ujenzi

| ENEO | ENEO LISILOZIDI META ZA ENEO ($M^2$) | VIWANGO VYA ADA |
|---|---|---|
| Eneo ambalo halijapimwa (unplanned settlements (special case) | 90-300 | 10,000/= |
| Kiwanja kilichopimwa Kidogo (high density) | 301-600 | 20,000/= |
| Kiwanja cha size ya kati ( Medium density) | 601-800 | 30,000/= |
| Kiwanja kikubwa ( Low density) | 801- 1200 | 45,000/= |
| Kiwanja kikubwa sana ( Super low density) | 1201- 2000 | 70,000/= |
| kujenga mnara ndani ya eneo la Halmashauri | | 500,000/= |

1. Ongezeko la ada kwa kila meta moja ya mraba zaidi ya meta za mraba 278.71 ni shilingi 150/=
2. Upanuzi wa majengo pia utafuata kiwango hiki

SEHEMU 'X': Ada ya maombi ya kusimika mabango ya matangazo ya biashara:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | 0.1 $M^2$ – 1$M^2$ | Tshs. 2,000/= kwa kila ombi |
| 2. | 1.1 $M^2$ – 2$M^2$ | Tshs. 4,000/= kwa kila ombi |
| 3. | 2.1 $M^2$ – 3$M^2$ | Tshs.6,000/= kwa kila ombi |
| 4. | 3.1 $M^2$ – 4$M^2$ | Tshs. 8,000/= kwa kila ombi |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | 1 $M^2$ – $5M^2$ | Tshs.10,000/= kwa kila ombi |
| 6. | 5.1 $M^2$ – nakuendelea | Tshs.25,000/= kwa kila ombi |

SEHEMU 'XI': Matangazo ya biashara 'promotion'

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Matangazo ya biashara kwa Wanyanyabiashara wadogo | Tsh. 20,000/= kwa siku. |
| 2 | Matangazo ya biashara kwa wanyabiashara wa kati | Tsh. 50,000/= kwa siku |
| 3 | Matangazo ya biashara Wanyabiashara wakubwa | kwa Tshs. 100,000/=kwa siku |

JEDWALI LA PILI

*(limetengenezwa chini ya Kifungu cha 5)*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO YANAYOZIDI TANI MOJA

Kibali kinatolewa kwa
Ndugu………………………………………………………………………….
Mmiliki wa Leseni au kitambulisho cha Mjasiliamali Na……………………………….
toka …………………………………
Kwa ajili ya kusafirisha mazao toka Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwenda
…………………
Kwa bidhaa yenye maelezo yafuatayo:

| Aina ya mazao yanayosafirishwa | Ujazo wa mazao | Ada na Ushuru uliolipwa Halmashauri | Na. ya risiti | Mahali mazao yanapotoka | Mahali mazao yanapopelekwa | Tarehe ya kusafirisha mazao |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |

Kibali cha kusafirisha mazao kimetolewa leo hii tarehe……….
mwezi………. mwaka………...

Jina la Afisa Mwidhiniwa……………………
Sahihi………………….

Cheo……………………
Jina la mwombaji wa
kibali……………………………………………………………
Sahihi…………………….
Tarehe…………………….

## JEDWALI LA TATU

*(limetengenezwa chini ya kifungu cha 13)*

## HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi ………………………………………………………… nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Bunda, kwamba tarehe …… ya Mwezi ………………. Mwaka ………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …………………………… cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda za Mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa faini ya kiasi cha shilingi laki mbili pamoja na Ada au Ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi……… Mwaka ……………………….

Jina……………………………………

Saini………………………………

Mbele ya:

Jina: ……………………………………………

Cheo: ………………………………………….

Saini: …………………………………………